TANGAZO LA SERIKALI NA. 655 la tarehe 8/9/2023

SHERIA YA KODI YA MAPATO,
(SURA YA 332)

# AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 10)*

AMRI YA MSAMAHA WA KODI YA ZUIO KWENYE RIBA YA MIKOPO KUTOKA TAASISI ZA KIFEDHA ZA NJE KATIKA MRADI WA UZALISHAJI MBOLEA ZA ASILI KWA KAMPUNI YA ITRACOM FERTILIZER YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Kodi ya Zuio kwenye Riba ya Mikopo Kutoka Taasisi za Kifedha za Nje Katika Mradi wa Uzalishaji Mbolea za Asili kwa Kampuni ya Itracom Fertilizer ya Mwaka 2023.

Msamaha

2. Kodi yote ya zuio kwenye riba ya mikopo kutoka taasisi za kifedha za nje kwa ajili ya mradi wa uzalishaji mbolea ya Kampuni ya Itracom Fertilizer inasamehewa.

Ukomo

3. Amri hii itafika ukomo tarehe 2 Julai, 2024 na inaweza kuongezewa muda kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa utekelezaji baina ya Kampuni ya Itracom Fertilizer na Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa tarehe 5 April, 2022.

Dodoma,
25th August, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*